**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*03 Julai, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS CHAPO AFUNGUA SABASABA, AZITAKA TANZANIA NA MSUMBIJI KUJENGA DARAJA LA BIASHARA

Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Mheshimiwa Daniel Francisco Chapo, leo ametoa wito kwa bara la Afrika kutumia biashara, viwanda na miundombinu yake ili kujenga uhuru wa kiuchumi na kuongeza thamani ya rasilimali zake.

Rais Chapo ameyasema hayo leo wakati wa ufunguzi rasmi wa Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, yaliyofanyika katika Viwanja vya Maonesho vya Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Rais Chapo yupo nchini kwa ziara ya kikazi kwa mwaliko wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Rais Chapo amesema pia Tanzania na Msumbiji zina nafasi ya kuwa daraja muhimu la biashara kati ya nchi za Afrika Mashariki na za Kusini Afrika, kwa kuendeleza fursa za ushirikiano katika nishati, kilimo, madini, utalii, uchumi wa buluu, viwanda, teknolojia, usafirishaji na biashara ya mipakani.

Fursa hizo, amebainisha, zinahitaji miundombinu imara, gharama ndogo za biashara, mifumo rahisi ya mawasiliano mipakani na minyororo ya thamani inayounganisha masoko ya kikanda na kimataifa.

Amesema bandari za Dar es Salaam, Mtwara zilizopo nchini Tanzania, Pamoja na Pemba, Nacala na Beira zilizopo Msumbiji, zinapaswa kufanya kazi kwa ufanisi na ushirikiano, badala ya kushindana, ili kukuza fursa za biashara na uchumi katika bara la Afrika.

***"Tanzania ni Msumbiji, na Msumbiji ni Tanzania. Kabla ya kuwa washirika wa kiuchumi, tulikuwa wenza katika mapambano ya ukombozi; na sasa wajibu wetu ni kubadilisha mipaka yetu kuwa korido za maendeleo na ustawi,"*** amesema Rais Chapo.

Vilevile, amewataka wafanyabiashara na wawekezaji wa Tanzania, Msumbiji, Afrika na dunia kuziangalia nchi hizo mbili kama eneo salama, la kuaminika na lenye fursa za uwekezaji wa muda mrefu.

Rais Chapo pia amewaalika wafanyabiashara wa Tanzania kushiriki Maonesho ya 61 ya Biashara ya Kimataifa ya Maputo (FACIM 2026), yanayotarajiwa kufanyika nchini Msumbiji, Mwezi Agosti mwaka huu.

Kwa upande wake, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema, kwa muda mrefu hadi sasa, Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yamekuwa jukwaa muhimu la biashara linalowaunganisha wazalishaji na wanunuzi; wafanyabiashara na masoko; pamoja na wawekezaji na fursa.

Amesema, kwa miaka 50, maonesho hayo yamechangia kukuza sekta binafsi, kufungua masoko kwa wajasiriamali, wakulima na wabunifu, pamoja na kuimarisha nafasi ya Tanzania kama lango la biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki, Kusini mwa Afrika, bara la Afrika na dunia kwa ujumla.

Rais Dkt. Samia amesema ushiriki mkubwa wa makampuni kutoka ndani na nje ya nchi unaonesha imani ya wawekezaji kwa Tanzania kama kituo bora cha biashara, uwekezaji, usafirishaji na ugavi katika ukanda wa Afrika.

Ameongeza kuwa, Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam yanapaswa kuendelea kutumika kama jukwaa la kugeuza uhusiano wa kihistoria kati ya Tanzania na Msumbiji kuwa fursa za biashara, uwekezaji, viwanda na ajira.

***"Wajibu wetu ni kuiendeleza historia hii na kuhakikisha haishii kwenye kumbukumbu pekee, bali inatafsiriwa katika uzalishaji, biashara, uwekezaji, viwanda, ajira, usafirishaji na ustawi wa watu wetu,"*** amesema Rais Dkt. Samia.

Akizungumzia uhusiano kati ya Tanzania na Msumbiji, Rais Dkt. Samia amesema uhusiano huo unapaswa kutoa matokeo yanayoonekana katika biashara, viwanda, ajira na ustawi wa wananchi, sambamba na historia ya ukombozi na ujirani mwema uliowekwa na waasisi wa mataifa hayo.

Amesema uwepo wa Rais Chapo kama Mgeni Rasmi umeongeza uzito wa kibiashara na kidiplomasia katika maonesho hayo, huku Tanzania na Msumbiji zikipewa nafasi ya kuendeleza udugu wao kupitia biashara, viwanda, uwekezaji na ajira.

Maonesho hayo yamewaleta pamoja washiriki kutoka Tanzania, Msumbiji na nchi nyingine, yakilenga kuimarisha biashara ya kikanda, kuvutia uwekezaji na kupanua nafasi ya Tanzania katika mnyororo wa thamani na ugavi, wa Afrika na dunia kwa ujumla.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu